Hadithi Ya Injili

Hadithi ya Mungu ni nini?
Kila mtu ana hadithi, nafikiri kwamba kila mtu ana hadithi, na ninafikiri kila mtu anaamini hadthi ambazo zinaeleza maisha yetu ieleweke vizuri. Hivi vinaitwa 'hadithi za kitamaduni' Lakini kama binadamu, tuko wadadisi, na tunataka tugundue majibu ya maswali kama vile, *'Tulikujaje duniani, na tunafanya nini hapa? Kusudi letu duniani ni nini, kama kweli kuna kitu kama kusudi?* Tunatamani furaha na faraja pia, na kila mara tunatafuta njia zote za kuboresha hali ya binadamu, kwasababu katika kilindini ya moyo, tunajua kwamba kuna kitu kibaya na kuwa ulimwengu huu unaonekana imepasuka mahali. Haijalisi kama kwamba hadithi yetu imebeba maneno kama 'dhambi' ama 'zenye kasoro', inaonekana kwamba tunafahamu kuwa ulimwengu huu haiko sawa. Jitihada imefanywa kujaribu kujibu maswali haya ya kina.

Dini nyingi, falsafa, majukwaa za kisiasa, na mitazamo yameshugulikia swala hili; zingine zimechangia kuboresha, lakini zingine zimezidi kuua na kuharibu. Ijapokuwa mjadala bado inaendelea, kuhusu ni nani ama ni nini inajibu maswali ya binadamu kwa ukamilifu, hadithi hi ni juhudi yetu tuwape hadithi ya Mungu katika mtazamo ya kibiblia na katika hali yetu ya karne ya ishirini na moja. Hivi ndivyo **Tuna amini;**

Tuna amini kwamba *"*Hapo *mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi,"* na kwamba uumbaji huo ulikuwa dhihirisho ya kisanii ya utukufu ya utatu ya hali Yake. (Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu), kwa kulitimiza *"Kusudi lake Jema"*. (**Mwanzo 1:1-2; Wakolosai 1:15-17; Waefeso 1:3-14**). Chochote Mungu alinena ikaumbika, na iliyoagizwa na amri Yake. (**Mwanzo 1:3-31; Isaya 55:11**). Mungu ki asili aliviumba vitu kutotumia chochote (Ex-Nihilo), na utaratibu kutoka kwa mchanganyiko, ambayo bado tuna amini anaendelea kufanya kupitia Neno Lake katika kila jambo. Wakati wa uumbaji huu haina maana kama ukweli ya kwamba kila kitu tunachokiona kiliumbwa papo hapo (bila kutumia chochote) katika Neno Lake, na kwamba *"na kwa uwezo Wake na kwa ajili Yake … vitu vyote vinahusiana kwa mpango"* (**Wakolosai 1:17**), na *'Tunaishi na kuenenda na kuwa na uhai ndani yake,'* (**Matendo Ya Mitume 17:28**). Chochote Mungu aliumba ilikuwa 'Njema,' ijapokuwa binadamu, ambaye alikuwa *"Njema Sana"* (**Mwanzo 1:3-31**). Hakuna kitu kilichoumbwa kilikuwa na uovu ndani, na chochote Aliumba ilikuwa kwa *'Utukufu Wake'* (**Isaya 43:7**) na kwa ajili ya "*Wema ya mapenzi Yake"* (**Waefeso 1:5,6,11,12,14**)! Hamna chochote Anahitaji wala deni lolote kutoka kwa vitu vyote alivyoviumba kabisa. Kwasababu Mungu ndiye muumbaji wa vitu halisi/viumbe hai, tuna amini kwamba Mungu Ndiye, "Kiumbe hai ya lazima" au 'Sababu isiyosababishwa," na haiwezi zuiliwa na viwango vya binadamu kama muda na nafasi ama visababu vinavyo sababisha vitu vitendeke, na ni kiumbe ya milele Ambaye ni tukufu (Tofauti na Alivyoumba) na ni binafsi (Ki Ungu na katika uweza wa enzi Yake Kuu Anashungulikia Uumbaji Wake). Utatu wa Uungu wote (Baba, Mwana na Roho) Wana utofauti kila mmoja, lakini wanaungana katika asili/kiumbe. Ingawa ni wazi kwamba kuna utiifu katika utatu wa Uungu, ni wazi kuwa kuna umoja (**1 Wakorinthia 11:1-3; Waebrania 5:8; Yohana 5:19);** na wote katika utatu wa Uungu wanashugulika na 'Kazi' ya Mungu, pamoja na uumbaji na wokovu (**Mwanzo 1:1-2; Waefeso 1:3-14**). Mungu Baba ndiye mbunifu, Mwana ndiye mtekelezaji na Roho Mtakatifu ndiye nguvu na uwepo Anaye thibitisha kuwa mpango

huo umefaulu kwa utukufu Wake, ili hatimaye viumbe vya Mungu vifurahi. Tuna amini kwamba ufahamu huu wa utatu wa Uungu ndiyo msingi kwa ajili ya jamii yote ya biblia (Katika kila muundo yake) na kwamba Mungu ameijenga umuhimu ya jamii katika asili ya kila binadamu, na ni muhimu tukaige mfano ya utatu wa Uungu katika miundo yote ya familia Mungu ameviumba (Familia ya binadamu, familia ya asili, familia ya Kiroho), kusababisha umoja thabiti katikati ya watu wana utofauti kubwa (**Waefeso 2:8-3:10; 4:11-16; Wafilipi 1:5,7,27; 2:2; 4:1-2**).
Tuna amini *kwamba "Mungu akaumba mtu* (binadamu) *kwa mfano wake; naam, kwa mfano wake Mungu alimuumba. Aliwaumba mwanamume na mwanamke"* na huyo mtu akawezeshwa ili waka *"Zaeni muongezeke, mkaijaze nchi na kuimiliki* (Kuilinda kutokana na maovu)*"* na *" Ailime na kuitunza "* (**Mwanzo 1:26-31; 2:15**). Kusudi ya kuumba binadamu ilikuwa ni kulima Utukufu wa Mungu na kuzalisha sifa ya Mungu vile inavyo "Zidishwa" (**Mwanzo 2:5,15**). Binadamu aliumbwa ili aridhishwe katika utukufu wa Mungu, na akaishi vile moyo wake umeridhishwa. Mungu alimpa binadamu chochote alihitaji kuendelea kuishi na kusitawi kama utamaduni yake (uwezo ya kuona, akili ya busara, ubunifu, chakula, maji, urembo, nk.). Mtu aliumbwa kwa mfano wa Mungu (wote wawili mwanamume na mwanamke), ambayo ndiyo tabia ya utatu ya Uungu vile inafanana ijapokuwa ni tofauti, umeunganishwa, na ijapokuwa kila mmoja wazi kivyake. Kwa hivyo upotovu yoyote kuhusu umoja huu ni udhalisaji ya kusudi la uumbaji na utofauti wazi Mungu alikusudia, kwa sababu utofauti wazi katika umoja inadhihirisha sura Yake katika ulimwengu huu. Na ni *"Ndiyo maana mwanamume humwacha baba yake na mama yake, akaambatana na mkewe, nao wawili huwa mwili mmoja."* (**Mwanzo 2:23-25**). Uumbaji ya utofauti wazi huo pia inaonyesha "Umwingine" wa uumbaji ambayo ni ujenzi ambayo inadhihirisha bora zaidi upendo na huruma, na inaonyesha uhusiano ambayo utatu wa Uungu unahusika nayo kikamilifu kwa kila mmoja. Pasipo utofauti wazi, hamna upendo wa kweli na huruma. Ijapokuwa wengi wanaona utofauti wazi kama ni uovu, na msingi ya vita na mzozo (mataifa, jinsia, jamii tafauti tofauti, nk.), tunaiona maonyesho ya uumbaji ni kama tamanio ya Mungu ya kuonyesha usanii Wake mbalimbali, na ni jambo njema pamoja na vitu vyote vilivyo umbwa.

Pia tuna amini kwamba Mungu aliumba mwanamke ili asaidie bwanake kutekeleza amri ambayo Adamu alipewa ya *"Kulima,"* utamaduni ya kumtukuza Mungu, na kwamba ijapokuwa wako sawa kabisa ki asili wanaonyesha utatu wa Uungu kwa kuwa wanafanana, ijapokuwa wana utofauti, na walionyesha utiifu na majukumu tofauti ambayo yanatekeleza amri kwa njia ya kuleta utukufu (**Mwanzo 2:1-15; 1 Timotheo 3:13-14; 1 Wakorinthio 11:1-3; Waefeso 5:22-31**).
Tuna amini kwamba kabla dhambi kuingia katika jamii ya binadamu, watu walikuwa na amani kamilifu (Shalom) na Mungu (Theolojia), na kila mtu na mwenzake (Sosiolojia), na wenyewe kwa wenywewe (Saikolojia) na mazingira yao (Ekolojia), iliyowawezesha wakuwe kamilifu ndani Yake, na kufurahi na kuabudu Mungu kamilifu vile walivyoumbwa wakafanye; ku *"Tangaza sifa zangu"*. Walikuwa kamili, na walikuwa na shalom kamilifu (Amani) na furaha katika kuabudu muumba wao, na kwa hivyo waliridhika na walikuwa kamilifu, pasipo kutamani zaidi ya yale walipewa.

Tuna amini kwamba licha ya amani huu, mtu alijaribiwa na Malaika walioumbwa na Mungu na wakamuasi ili wawe miungu wao wenyewe; wakatenda vitendo na kufuata misukumo yao zilizowaweka waonekane wakubwa kuliko Mungu kwa ajili ya kujitukuza wenyewe (tazama **Isaya 14**).

Hili jambo halikufanyika nje ya uangalifu ya Mungu au nje ya mpango Yake, lakini baada ya muda, mtu *"Kwa maana watu wangu hawa wametenda maovu mawili; wameniacha mimi, niliye chemchemi ya maji ya uzima, wamejichimbia visima, visima vyenye nyufa visivyoweza kuweka maji."* (Yeremiah 2:13). Ilikuwa ni kiburi hii ndani ya moyo wake ndiyo ilileta janga hili, na matokeo ya baadae ya kuanguka kwa watu wote iliyosababisha moyo wa binadamu ikuwe *"Mdanganyifu kuliko vitu vyote"* na imekufa kiroho ndani **(Yeremia 17:9)**. Kiini cha dhambi ya Adamu ilikuwa ibada ya sanamu na kiburi iliyopitishwa kwa wanadamu wote. Hii ilisababisha mtu akuwe katika hali ya kustahili ghadhabu ya Mungu na hukumu, kwa sababu katika kutotii kwake, moyo wake (Kiini cha Motisha) ikawa *"Mdanganyifu kuliko vitu vyote"* na ana uwezo ya kutenda kila aina ya uovu. Hukumu basi ni kutekeleza haki kamilifu kinyume na uasi huu, na hamna mtu yeyote ana udhuru (**Warumi 1-3**). Hatimaye watu wote wanazaliwa na asili ya kutaka wakuwe Mungu wao wenyewe na wamekufa kwa ajili ya Mungu na kwa ajili ya ujumbe Yake ya wokovu pasipo kuzaliwa mara ya pili kwa uwezo wa Roho Mtakatifu katika maisha yao (**Mwanzo 3:5-6; Warumi 5:12**). Mtu anaonyesha hii hali yake ya kufa ama kwa kujitengenezea maisha imejawa raha pasipo na Mungu, au maisha ya kidini/wema nje ya mapenzi ya Mungu ili akatawale wokovu/hatima yake mwenyewe (Tazama **Luka 15:11-32**). Kwa kozi yoyote, binadamu amekataa Mungu asiwe kama "*Chemchemi ya Maji ya uhai*" na wakajiundia taratibu yao ya wokovu ambayo hayatimizi shauku yetu ya kuabudu, na wametulia kuabudu miungu (Ambayo ni kuabudu sanamu) wakijaribu kukidhi nafasi ulioachwa kwa kuweka miungu iliyosababishwa na kukataa Mungu (**Yeremia 2:13; Yohana 7:37-39**). Kwa hivyo tumelaaniwa kwa sababu ya matendo yetu mbaya, pamoja na matendo yetu mema, na kuhitaji vibaya sana mwokozi (**Waebrania 6:1**). Ni hii hali ya kukataa Mungu na kusababisha kuabudu "miunngu" imeacha binadamu bila kurithika na akitamani zaidi, ambayo yameleta udhaifu kila mtu anapitia mara kwa mara (Vita, ubaguzi wa rangi, uchungu, kutosamehe, itikadi kali ya kidini, kashfa, ulafi, tabia mbaya zote za ngono, dhuluma, nk).

Tuna amini kwamba matokeo ya dhambi hii ni madhara mabaya na janga inasababisha kuvunjika na uharibifu ya ki theolojia, sosiolojia, saikolojia na ya kikolojia. Shalom ya binadamu imeharibiwa na watu wanaendelea kutafuta kwa wingi "Visima vyenye nyufa" ili wajaze shimo ndani ya nafsi yao, na inazidi kuleta janga duniani tunapoendelea kutafuta maana na furaha nje ya kusudi ya uumbaji wetu; ambayo ni kuabudu Mungu wa milele. Mtu anaendelea kuabudu, lakini kwa bahati mbaya anapendezwa na mambo haraka, na anaingiana na suluhu nyingi ambayo *"Ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, Lakini mwisho wake ni njia za mauti."* (**Mithali 14:12; 16:25**). Shida za binadamu haziwezi kusuluhishwa na maadili za mikataba, saikolojia ya binadamu, tiba, huduma ya jamii, uhisani, utajiri, elimu, taasisi za kibinadamu, nguvu ya kijeshi, kidini au kisiasa. Hata hivyo binadamu, wanapokataa Mungu wanaendelea kuunda mbinu ya shalom kutokana na kiburi na kuabudu kwao sanamu, ambayo hayaridhishi, na hatimaye matokeo yake ni kutoridhika na mauti. Hata hivyo, Mungu katika neema yake Alianza kushambulia uovu, kwa kuweka kikwazo katika maisha ya binadmu na kuleta kifo ya kimwili pamoja na kifo ya kiroho kama matokeo ya uasi huu. Huu neema uliweka kikwazo katika uwezo wa binadamu ya kuunganishwa chini ya muundo wa utawala wa ubinafsi (**Mwanzo 2:17; 11:6-7**). Ijapokuwa binadamu anajitahidi kuwa na umoja, kila mara wanagawanyika, kwa sababu kiburi na uoga unaharibu uhusiano, na huleta vita; kibinafsi na kwa watu wengi (**Yakobo 4:1-3**). Hata kama watu wengi wanaamini kwamba shida ni utofauti wetu, injili inatukumbusha kwamba ni mioyo yetu wenyewe imejaa dhambi, na kwamba utofauti katika waliokombolewa ndiyo unaleta upendo na huruma na dhamana ya kweli. Kwa hivyo tuna amini kwamba "wokovu" sio tu "kuokoa" watu, lakini ni kukomboa viumbe (**Warumi 8:19-25**), na hali ya mwili yetu yenyewe. Suluhisho ya kibinadamu bado inaendelea kuwa ni ama kukomesha tamanio au utofauti kupitia kwa kulazimishwa, ilhali injili ubadili mioyo, na kuumba kipya mtindo ya wazo mabaya ya dhambi ya mantiki ya binadamu, na kurejesha viumbe vya Mungu vile Alivyo kusudia ikuwe. Kwa hivyo tuna amini kwamba Yesu, ambaye ni Mwana wa Mungu wa milele *"Bali alikubali*

*kuacha vyote, akachukua hali ya mtumishi, akazaliwa na umbo la wanadamu. Alipochukua umbo la mwanadamu, (*Pasipo kupoteza asili Yake ya Uungu) *alijinyenyekeza akawa mtii mpaka kufa,*" ili akatekeleze kikamilifu mapenzi ya Baba, *"tena kifo cha msalaba."* (**Wafilipi 2:7-8**), iliyo pangwa hapo awali *"Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu"* (**Waefeso 1:4; Waebrania 4:3**). Yesu akawa mbadala yetu mkamilifu kwa sababu hata yeye alikuwa mtu (Kwa hivyo akachukua adhabu yetu ya machafuko/dhambi, na alikuwa ni Mungu (Akiwa kamilifu ya kutosha kulipa dhambi zetu), ambayo ilimwezesha pasipo dhambi kutupatanisha kwa ajili ya makosa zetu na kutupatia haki Yake, ambayo ilihitajika iwe haki ya kutosha ya kuwezesha mtu aingie katika uwepo wa milele wa Mungu mtakatifu na wa haki. *Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu* (**2 Wakorinthio 5:21; 1 Petro 2:24**).

Tuna amini kwamba Mungu anahukumu binadamu kwa haki kwa sababu ya uhaini wa ulimwengu huu, ijapokuwa katika neema Yake Aliahidi kutuma mwokozi kuponda dhambi na uovu, na kukomboa binadamu kutokana na hii anguko ya kuogofya. Halafu akaonyesha neema hii na dhabihu ya Kondoo dume na kufunika uchi wao, ilikuwa ni maonyesho ya ishara ya kuwa siku moja Atafunika dhambi zao, na damu Yake mwenyewe, ambayo iliahidiwa na Mungu kuharibu uovu kupitia *"Uzao wa mwanamke"* (**Mwanzo 3:15,21; 22:13-14; Kutoka 12:42-51; Waebrania 9-10**). Ingawa haieleweki kamilifu uovu asili ilitendeka katika bustani ya Edeni, na mapenzi ya mtu katika anguko hii, tunafahamu ya kuwa Mungu Ndiye Mkuu, na hakuanzisha uovu. Kwa upande mwingine, tunajua kwamba Yeye ndiye *"Mimi naiumba nuru, na kulihuluku giza; mimi nafanya suluhu, na kuhuluku ubaya"* **(Isaya 45:7).** Licha ya Mungu kuwa kabisa ni mkuu zaidi (hata hivyo hakuanzisha uovu), mapenzi ya mtu haikosi katika uamuzi huu. Dhambi ilitokea kupitia tamaa na chaguo ya mtu, na Mungu anabaki mwenye haki anapo hukumu binadamu kwa sababu ya uasi na kiburi yetu. Pia tuna amini kuwa, *"Kwa njia ya mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, nayo ikasababisha kifo,"* kwamba, *"Lakini ipo tofauti: neema ya Mungu si kama dhambi ya Adamu. Maana, ingawa dhambi ya mtu mmoja ilisababisha kifo kwa wote, kwa fadhili ya mtu mmoja, yaani Yesu Kristo, Mungu amewazidishia wote neema na zawadi zake"* (**Warumi 5:12-15**). Kama vile dhambi iliingia kupitia mtu mmoja, wokovu pia inakuja kupitia kazi ya mtu (Yesu) mmoja msalabani.

Kisha tuna amini kwamba *"Wokovu ni ya Bwana,"* na ambaye Mungu *"Aliowachagua tangu mwanzo, ndio Aliowateua wapate kufanana na Mwanae"* (**Warumi 8:29**) na *"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; na si kwa sababu ya matendo yenu mema. Hii ni zawadi kutoka kwa Mungu mwenyewe. Na kwa sababu hamkuifanyia kazi, mtu ye yote asije akajisifu juu ya wokovu wake"* (**Waefeso 2:8,9**). Wokovu wetu kwa ukamilifu na kabisa inategemea kazi ya Bwana wetu. Hadi mioyo yetu iliyokufa izaliwe mara ya pili kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, hatuwezi "Kujichagulia" Mungu sisi binafsi (**Mathayo 15:12**). Kila mara tunaunda dini na mila ya dini tukijaribu kukidhi miungu zetu za aibu na uoga, likini hatuwezi kuja kwa Yesu *"Baba aliyenituma asipomvuta"* sisi na kutupatanisha na Mungu kwa ajili ya dhambi zetu *(***Yohana 6:44**). Hata hivyo hii haipunguzi mapenzi ya binadamu, lakini inaielekeza chini ya ukuu ya mapenzi ya Baba, ambaye bado anataka kila mtu aitikie vyema injili (**Warumi 10:13-15;** tazama **Yohana 1:12,13**), ambayo huwezi kuzuia wakati nguvu za Roho Anayewezesha moyo wa mtu uliokufa uzaliwe upya. Tuna amini kwamba Mungu ana kila haki ya kuita watu kupitia Mwanae, na kwamba yeye ni wa haki pamoja na kutukuzwa kabisa kupitia wale wanao pata uzima wa milele katika Yeye, na wale wanao hukumiwa katika laana ya milele. Moja inasisitiza upendo na rehema ya Mungu, na ya mwisho inaonyesha haki na utakatifu Wake. Mungu hatoi hukumu kwa yeyote kwa njia isiyo ya haki, pia hawezi kuruhusu mtu yeyote mbele zake kwa njia isiyo ya haki. Kila mmoja wetu anaelekea hukumuni, kwa hivyo Mungu ni wa haki katika kila tendo Lake. Pia tuna amini kwamba hukumu ya milele ya Mungu ni haki Yake ya milele kwa ajili ya mabaya yote mengi yametekelezwa na uovu katika historia yote. Pasipo hukumu baada ya kifo itasababisha maisha hii ikose maana, na

ukatili na makosa tunazoziona katika ulimwengu huu ionekane kama haina maana. Kwa hivyo tuna amini, kwamba ili Mungu Awe wa haki kwa kweli, ni lazima ahakikishe kwamba adhabu ya dhambi, ambayo ni mauti, imelipwa kulingana na sheria alipeana kwa watu Wake. Kwa hivyo ingawa ni kweili kwamba "*Wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu*" (**Warumi 3:23**) tuna *"Kufanyika wenye haki* (Bure) *kama kipawa kwa neema Yake kupitia ukombozi katika Kristo Yesu, Ambaye Mungu Alidhihirisha wazi kama mpatanishi katika damu Yake kupitia imani"* (**Warumi 5:15-17**), ambayo "*Kuonyesha kuwa hutenda haki Alikuwa sahihi huko nyuma alipovumilia na hakuwaadhibu watu kwa sababu ya dhambi zao*" (**Warumi 3:25**). Halafu Mungu ni wa haki kabisa katika matendo Yake Kristo ya kuokoa binadamu, pamoja na, kuwahukumu kwa ajili ya dhambi yao wakikataa njia Yake moja ya kipekee ya wokovu ambayo ni mzuri sana kwa ajili ya uhalifu wetu. Kwa hivyo, Kristo ni "*Mwokozi wa watu wote, hasa wa wale waaminio*" (**1 Timotheo 4:10**) kufanya kazi Yake msalabani kutosha kwa watu wote, na bado ni ufanisi kwa wale wanao tumaini kwa hii kazi ya wokovu. Mungu ni wa rehema na mtakatifu, na Hawezi kudhihakiwa.

Tuna amini kwamba Kristo hakulipa tu adhabu ya dhambi yetu, lakini kwamba *"yeye ambaye hakujua dhambi, awe dhambi kwa ajili yetu ili ndani yake tupate kuwa haki ya Mungu"* . Haki yetu basi ni Yake, na sio yetu binafsi, inawapa wale wanao Mwamini hali ya ukamilifu mbele ya Mungu mtakatifu na wa haki. Tunapo anza kutambua vile Mungu ni mtakatifu na vile tuko na dhambi kuu sana, msalaba inakuwa kubwa sana katika maisha yetu, na tunakuwa na uwezo ya kuishi maisha imejawa neema na wale wanaoishi karibu nasi. Tunapewa motisha na upendo wa Mungu ya kupenda wengine na tuna anzisha huduma ya kupatanishwa ambayo tulipewa na Baba kwa ajili ya utukufu Yake (**Mathayo 22:37-39; 2 Wakorinthio 5:17-21**). Hii pia inatusaidia tuwe watu wa kutubu kwa sababu tunachukia dhambi yetu, sio kwa sababu tuko na hatia au tunajaribu kuendesha Mungu atufanyie jambo, lakini ni kwa ajili ya upendo Wake kuu kwetu. (**Yohana 3:16; Warumi 5:8; 1 Yohana 4:8-11**). Tunapoishi katika neema, tunakuja kugundua kwamba tunastahili kutubu kwa ajili ya "*Kazi zisizo* (Mzuri) *na uhai*" (**Waebrania 6:1**) kama vile kazi zetu mbaya, na kwamba dhambi zetu sio lazima ikuwe kitu tunatenda, lakini zinathihirisha hali ya moyo ambayo imekataa Mungu kwa njia mbali mbali pamoja na kujitoa kidini, ambayo, pasipo kukombolewa kwa moyo, inaweza unda moyo ya haki ya kujitegemea binafsi au ya uchungu (Motokeo ya dini pasipo Yesu). Akili ya kidini inaendelea kufikiri kwamba dhambi ni swala la mambo ya nje, na suluhisho ziko ndani, na kwamba tunakubalika kupitia matendo yetu, ijapokuwa injili inatuonyesha kwamba dhambi iko ndani, na suluhisho iko nje (Yesu), na kukubali kwetu iko katika kazi Yake, na kwa hivyo tunaweza Kumtukuza Katika kazi zetu kama matokeo. Basi ni kwamba "*Sicho kiingiacho kinywani kimtiacho mtu unajisi; bali kitokacho kinywani ndicho kimtiacho mtu unajisi…. vitokavyo kinywani vyatoka moyoni; navyo ndivyo vimtiavyo mtu unajisi. Kwa maana moyoni hutoka mawazo mabaya, uuaji, uzinzi, uasherati; wivi, ushuhuda wa uongo, na matukano; hayo ndiyo yamtiayo mtu unajisi*" (**Mathaayo 15:10-20**). Matendo yetu hatimaye ni dalili ya hali mbaya ya moyo, huwa "*Mdanganyifu kuliko vitu vyote, nani awezaye kuujua?*" (**Jeremiah 17:9**). Ni mageuzi ya Roho Mtakatifu peke yake, na nguvu Yake ya kuzaliwa upya ambayo inaweza kubadilisha hii moyo wa jiwe, na Akaweke ikuwe "*Moyo wa nyama*" (**Ezekieli 36:25-30**). Basi tuna amini kwamba simulizi ya Mungu (Biblia) inatukumbuza kwamba Mungu Atahukumu uovu kikamilifu na kwa haki, na kwamba Ako kwenye kazi ulimwenguni Akipatanisha ulimwengu kwake Mwenyewe. Hata hivyo hata katika hukumu ya haki, Yeye Anapata " *Hapendezwi na kifo ya mtu yeyote.*" na Anatamani kwamba wote '*'Watubu na kuishi"* (**Ezekieli 18:32; 2 Petro 3:9**). Alianza ki maono kazi ya ukombozi kwa kuita watu Kwake Mwenyewe kwa kusudi Lake na utukufu Wake mwenyewe. Kwamba hawa watu wangekuwa *Baraka kwa jamaa zote za dunia*" (**Mwanzo 12:1-4**) na itakuwa ni jukumu la watu Wake wiliokombolewa kutimiza "*Zaeni, mkaongezeke*" na kuonyesha utukufu Wake katika ulimwengu yote.

Baadae Mungu Akaita Ibrahimu akue Baba wa mataifa, na kuelekeza kwa Mungu kama Mwokozi wetu wa pekee. Licha ya wema wa Mungu kwa binadamu, watu walizidi Kumkataa na kuikiuka sheria Zake, wakililia uongozi ya kiulimwengu, badala ya kujiweka chini ya utawala wa ukarimu wa Mungu Mkuu. Binadamu aliendelea kuonyesha matokeo yake ya moyo wa uasi, na akashindwa kumtukuza Mungu, ili awe mshuhudaji wa utukufu Wake (Tazama kitabu cha **Waamuzi 21:25; Warumi 3:23).** Kwasababu binadamu anaendelea kumuasi Mungu na kutamani kujiokoa wenyewe, Mungu Akaonyesha Ibrahimu na ukoo wake na manabii, kwamba dhabihu itahitajika ya kulipa kamilifu adhabu ya dhambi zetu, na kwamba dhabihu ya mnyama (Ijapokuwa ni Ishara), haingelipa kikamilifu adhabu ya janga hili la uharibifu, lakini kungekuwa na dhabihu ambayo ingeharibu dhambi na aibu milele (**Yohana 1:29-36**), na kusababisha utiifu kutoka kwa moyo mpya na sio matendo ya kitamaduni ya dini ya kutoa dhabihu na wajibu, kwasababu ni *"Kutii ni bora kuliko dhabihu"* (**1 Samueli 15:22**). Tendo Lake kuu ilikuwa ni kutuma Mwanaye ili Awe dhabihu ya mwisho, mara moja na kwa wote, ambayo ingeshinda dhambi na kifo, kwa kumfufua kimwili kutoka mautini, kwa uweza wa Roho Mtakatifu, Akamweka Awe wa pekee *"Jina duniani ambalo wamepewa wanadamu, peke yake tunaweza kuokolewa"* (**Matendo Ya Mitume 4:12**). Kwa hivyo, kwasababu ya ufufuo, tunaamini kwamba hakuna njia nyingi za kuelekea mbinguni, lakini kwamba Yesu Ndiye *"Njia na Kweli na Uzima; mtu hawezi kufika kwa Baba bila kupitia kwa Yeye"* (**Yohana 14:6**). Wazo ya kwamba njia zote zaelekea kwa Mungu (miungu), ni kivyake usemi ya dini ambayo ni ya wenye kushikilia maoni bila msingi na ni kinyume na sheria ya mantiki na ufunuo ya Neno katika milki yetu. Pia ni mtazamo wa ulimwengu ya upande unao egemea sana Magharibi imechafuliwa na upepo wa muktadha wao wenyewe na inakera kwa ukali sana tamaduni zingine. Hakuna taasisi yoyote ya binadamu imewahi kuwakilisha Mungu kikamilifu hapa duniani, lakini Yesu Aliita Kanisa Lake ndiyo ikuwe "Israeli mpya", na Bibi arusi Wake ili atembee pamoja Naye kwa ajili ya kutimiza utume Yake duniani (**Yohana 10:16; Waefeso 5:29-31; Warumi 9:6**). Hivyo hatuokolewi tu kwa nguvu ya injili, likini tunaokolewa pia kwa kutimiza "Kusudi" za injili, ambayo ni kazi ya utume ya Mungu duniani (Waefeso 1;10-11; Yohana 20:21). Hivyo Kanisa (Eklesia) ni walioitwa na kutengwa na kukombolewa na Mungu kama wamisionari ili wawe Baraka kwa mataifa, na washuhudaji katika "*Yerusalemu na Yudea yote na Samaria, hadi mwisho wa dunia*" (**Matendo Ya Mitume 1:8**). Kumbe injili ni Mungu kuvunja utamaduni ya binadamu ili akomboe kwa ajili ya utukufu Wake Mwenyewe, Kanisa imeitwa ikuwe sehemu ya utume hiyo, tunapo hubiri injili na kuishi katika maana yake kwa mtindo ya kumtukuza Mungu. Yale Mungu alianzisha, na akaona kwamba ni "Mwema", Anakomboa, na siku moja wakati Kristo atakaporudi mara tena kukomboa kamilifu uumbaji na kukabidhi *"Mji mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka kwa Mungu mbinguni. Ulikuwa umetayarishwa vizuri kama bibi arusi aliyepambwa tayari kukutana na mumewe"* (**Ufunuo 19:7,8:21:2**) na mapenzi Yake, *"Yafanyike hapa duniani kama huko mbinguni"* (**Mathayo 6:10**).

Yesu atarudi tena mara ya pili ili akamilishe aliloanzisha msalabani, na ufufuo Wake kutoka kwa wafu wa baadae, na kuanzisha Kanisa Lake, ambayo inabeba watu wote ambao Wanamwamini kwa ajili ya wokovu wao, wakitubu kwa ajili ya uovu wao na matendo yao mema, na Kumtambua Yeye pekee kama mwokozi wao, na hatimaye atatoa hukumu kwa "Walio hai pamoja na wafu", atakapo haribu uovu mwishowe, akikaribisha mbingu mpya na dunia mpya ambayo itakuwa imekombolewa kamilifu na imewekwa huru pasipo na uovu, na imejawa na uwepo na utawala wa Mungu. Kwa muda sasa Kanisa wako kama wateule wa Mungu kwa ajili ya utukufu Wake. Tunaona haya kwa kuwa, *"Ili sasa kwa njia ya Kanisa, hekima yote ya Mungu ipate kujulikana kwa watawala na wenye mamlaka katika ulimwengu wa roho"* (**Waefeso 3:10**). Watu wa Mungu, Kanisa, ndiyo washuhudaji kwa ulimwengu kuhusu urejesho wa kuvunjika, na uadui na chuki kwa uwezo wa Mungu. Mungu Anatukuzwawakati Kanisa inawakilisha nia ya Mungu kwa ulimwengu, ili ukuta ya mgawanyiko ya uadui ivunjwe katikati ya

binadamu na Mungu na binadamu na binadamu. Ubaguzi wa rangi, chuki, ubaguzi, na ibada za kutengwa ni matokeo ya dhambi na sio matokeo ya Roho Wa Mungu (**Waefeso 2:10-3:10; Wagalatia 2:14; Ufunuo 5:7-9; 9:7**). Kanisa Lake linaongozwa na mashemasi na wazee wa Kanisa (**1 Timotheo 3; Tito 1; Matendo Ya Mitume 14:23; 20:17-28**) wanao tunza Kanisa na kuchunga, kufundisha na kuhudumia. Tuko ili tuishi kwa ajili ya utume Yake na utukufu Wake (**Mathayo 28:19-20; Matendo Ya Mitume 1:8; 1 Petro 2:9**). Kanisa inasimama kwenye nafasi ya kutangaza hadithi ya Mungu hadi kurudi Kwake tena Bwana wetu Yesu Kristo, wakati sisi sote tutapokea miili za utukufu na tutadumu na Kristo milele tukimwabudu Yeye Ambaye tumeumbwa ili tumwabudu na tukapate furaha yetu ndani Yake. Kwa hivyo *"kuishi ni Kristo na kufa ni faida"* (**Wafilipi 1:21**). Katika kifo, hatimaye tunapata furaha ambayo tunajitahidi kupata hapa duniani. Kanisa itatukuzwa katika hii furaha, itakapo abudu Mungu kamilifu katika Kristo milele. Wakati tunaishi katika hali ya kuridhika hapa duniani tunapopata furaha katika vitu "Vyema"tumepewa katika maisha hii, hatuwezi kupata tumaini na furaha kamilifu katika hizo vitu, lakini tunapata katika Kristo, na tutapata hizo zote kamilifu katika hali yetu ya kuishi milele. Kabla ya hayo, tumepewa *arabuni ya urithi wetu, ili kuleta ukombozi* kupitia Roho Wa Mungu kama amana na ukumbusho ya neema Yake tunapoendelea kuishi maisha iliyovunjika katika dunia iliyovunjika (**Waefeso 1:13-14**).

Kwa hivyo tunaamini kwamba uzima wa milele ni kwamaba ili *"wakufahamu wewe ambaye pekee ni Mungu wa kweli, nakumfahamu Yesu Kristo ambaye umemtuma"* (**Yohana 17:3**), na kwamba tukona tumaini katika maisha haya kwamab Kristo Atarudi tena na kutawala pamoja na Kanisa Lake, akiota ibada ya watu Wake wanao mtukuza kupitia kuabudu asili Yake kwa njia inayoridhisha kabisa. Tunaamini pia Bwana wetu Atarudi upesi, na Atakomesha kabisa uovu, kifo na dhambi, na Atawale, pamoja na watu Wake katika mbingu mpya na dunia mpya milele. Kwasababu hiyo tunaamini kwamba mjadala kuhusu mpangilio na wakati ya kurudi Kwake Kristo haina manufaa sana, na imeshindwa kutambua kwamba Baraka yetu haipatikani katika maisha yetu ya baadaye, lakini inazidishiwa katika maisha yetu ya baadaye. Kristo Ndiye tuzo na hakuna vipawa vingine vinaweza kunyakua dhamana na kusudi la uhusiano ya kuabudu pamoja na Mungu kupitia Msalaba ya Yesu Kristo. Tunaamini pia kwamba ijapokuwa ahadi nyingi yametimia kwa kukuja Kwake Kristo mara ya kwanza, lakini sio zote zilitimia, na kwamba kuna vipengele vya Baraka Zake kama kuishi maisha pasipo kutenda dhambi, uponyaji pasipo kuwa mgonjwa tena, ukombozi kamilifu, kukosha machozi, nk. hazitaweza kutimia hadi Kristo Atakaporudi tena. Kwa hivyo tunasikilia wazo ya kwamba "Yametendeka/na bado" katika mafundhisho ya nyakati za mwisho, maanake ni kwamba tunakamilishwa "Katika Kristo", na hiyo ukamilifu itadhihirishwa tu wakati tutatukuzwa mwishowe wakati wa mwisho wa nyakati (**1 Wathesalonike 4:13-5:11; 1 Wakorinthio 15**).

Hadi hapo, bado tunaona hafifu katika kioo (**1 Wakorinthio 13:12**), lakini tunazidi kupata ufahamu tunapo tafakari Neno la ufunuo la Mungu, ambalo ni lenye faida kwa, *"Mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki"* (**2 Timotheo 3:16; Warumi 12:2**). Mungu pia ametoa kwa Kanisa vipawa vya neema na watu ambao wanatusaidia ili tukue katika umoja na ufahamu ya Yesu, na kuishi kwa ajili ya utukufu Wake **(Waefeso 4:11-13; 1 Wakorinthio 12-14; Warumi 12:3-9**). Pia, ijapokuwa tunaamini kwamba Mungu anaweza kutumia kipawa chochote Anataka kwa ajili ya Kusudi Lake na kwa Wakati Wake, na tunaamini kwamba Yeye Ndiye hupeana kila kipawa kamilifu kwa hiari Yake, ikiwa tayari na itubariki sana (**Yakobo 1:17**), tunakwepa "Injili ya mafanikio" kama ukweli nusu ambayo hatima yake ni uzushi, uchungu na/au haki binafsi. Inageuza mtazamo wetu ikuwe hatari ikitazama mlalo kama tuzo, na inachochea wazo kwamba Mungu ni njia tu kwetu ya kupata furaha, afya na mali hatimaye, ambazo Neno inasema zinapatikana kwa Mungu tu, na kwa ukamilifu tutakapomuona uso kwa uso. Binadamu amevunjika, na Mungu tu Ndiye chanzo cha furaha na uponyaji ambayo itadumu milele tangu sasa na ikiingia hadi milele na

milele. Tumeambiwa na Yesu kwamba katika ulimwengu tutapitia *Adha*, lakini ndani Yake tutakuwa na amani (**Yohana 16:33**), na mafundisho yoyote ambayo haifundishi kuhusu mateso sio ukweli wa Biblia, na imeshindwa kufundisha ushauri kamilifu ya ujuzi ya binadamu duniani. Kufahamu kwamba Mungu haondoi mateso yetu hapa duniani, lakini inatuonyesha kwamba Mwokozi wetu alipitia mateso yote tutapitia, na Yeye Ako pamoja nasi tunapopitia haya sasa (**Zaburi 23:4**). Pia inatufundisha kwamba tukona hatima kuu katika Kristo, hiyo inapunguza mateso tunapitia katika maisha haya (**2 Wakorinthio 4:7-18**).

Nifanyaje ili Yesu Kristo Aongoze maisha yangu (Yohana 3:16; Matendo Ya Mitume 2:37-38; 16:30-31; Warumi 3:23; 6:23; 10:8-15; Waefeso 2:8-9; Waebrania 11:6)

"Yesu Aliishi maisha hatungeishi na Akafa kifo tungekufa" **Lacrae**

Ijapokuwa tumeokolewa kweli na neema ya Mungu, na Yesu Amelipa gharama ya dhambi zetu msalabani, na hakuna kitu tuna "Fanya" ilitupokee wokovu, Neno ni wazi kwamba ni lazima *Tuamini* (Maanake ni kutegemea)Yeye kama wokovu wetu pasipo kutegemea mbinu zingine za wokovu, na kutangaza hiyo wazi kwa njia ya batizo na kuangama. **Warumi 6:23** inasema *"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu"* ambayo ni Baraka mno! Hatua hii uanza na **Toba** (Kutambua kwamba sisi ni wenye dhambi). Watu wengi wanajukwaa kwa ajili ya jambo hili, kwasababu hawahisi kwamba wameishi maisha "Mabaya", lakini dhambi sio tu yale tunatenda, lakini ni asili yetu katika kiini ya mioyo yetu. Hadi tukubali kwamba tumekataa njia za Mungu ili tukafuate njia zetu wenyewe, hatuwezi kumjia Mungu. Tumetengwa kabisa na Mungu, na hamna njia nyingine ya kuenda Kwake, lakini kupitia Yesu kwanza, kwa kukubali kwamba sisi ni wenye dhambi na tunahitaji wokovu. Ni muhimu hapa kutambua kwamba tunahitajika tukatubu kwasababu ya matendo zetu mema za kidini, pamoja na matendo zetu za uasi. Tukisatambua dhambi zetu, lazima **Tuamini** kwamba Kristo Ndiye Yule Anayesema ni Yeye, na kwa hakika Amelipa bei ya dhambi zetu! *Imani* ni kipawa cha Mungu kinachoanzisha neema ya wokovu Wake katika maisha yetu. Ni kwa imani tunampendeza Mungu. Halafu **Tubatizwe** kama kitendo cha utiifu kwa Yesu kama Bwana wa maisha yetu. Batizo haiwezi kutuokoa, lakini tumeamrishwa tubatizwe, kwasababu ni njia inaonekana wazi na hadhara kujitoa kwetu kwa Yesu kama Bwana wa maisha yetu. Katika batizo tunapokea Roho Mtakatifu Ambaye Anatuwezesha tukaishi maisha ambayo hatuwezi kuishi pasipo Kristo kukufa kwa ajili ya dhambi zetu, na Roho Anatuwezesha tukafanye hivyo.

Kwa mailezo zaidi andikia kwa theaiinitiative@gmail.com

Translated by Pastor Tom Opiyo, People For Jesus Ministry, Narok , Kenya, East Africa. Tel: 254-721-204447. Email: peopleforjesusintmin@gmail.com. Translated with permission from Michael Gunn, the author of the article.